# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

## TAMKO KUHUSU UCHUNGUZI WA KIFO CHA ND. ATHUMAN HAMAD ATHUMAN NA AMOUR KHAMIS SALIM WAKAAZI WA KIUNGONI WILAYA YA WETE MKOA KASKAZINI PEMBA WANAODAIWA KUFARIKI WAKIWA MIKONONI MWA MAOFISA WA MAMLAKA YA MADAWA YA KULEVYA PEMBA.

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) imepokea kwa masikitiko makubwa vifo vya Nd. Athuman Hamad Athuman na Amour Khamis Salim wananchi waliokuwa wakiishi katika kijiji cha Kiungoni. Kwa mujibu wa taarifa za vyombo vya habari na mitandao ya kijamii inadaiwa kuwa marehemu walichukuliwa na askari wa Mamlaka wa Kudhibiti Madawa ya Kulevya wakiwa wazima kwa tuhuma za kuhusika na wizi wa baskeli na matumizi ya bangi lakini walirejeshwa siku ya pili wakiwa wameshafariki.

Aidha, kwa mujibu wa taarifa kwa Umma ya Jeshi la Polisi Mkoa wa Kusini Pemba ya tarehe 25/12/2024 ilieleza kuwa Jeshi hilo linaendelea kufanya uchunguzi wa vifo vya watu wawili ambao walifariki dunia wakati wakipatiwa matibabu katika Hospitali ya Ali Khamis Camp Vitongoji Pemba. Taarifa hiyo imeeleza kuwa waliofariki ni Nd. Athuman Hamad Athuman miaka 75 na Amour Khamis Salim miaka 28 wakaazi wa Kimango Kiungoni Wilaya ya Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba, baada ya kukamatwa na Maafisa wa Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Madawa ya Kulevya Pemba wakishukiwa kujihusisha na madawa ya kulevya.

Kwa upande wa taarifa kupitia Mtandao ya kijamii iliyorushwa ikimuonesha mzee mmoja aliyejitambulisha kama mdogo wa marehemu Athumani Hamad Athuman alieleza kuwa yeye na wenzake walipata ujumbe kuwa wanatakiwa wafike katika Hospitali ya Chakechake na walipofika huko waliwakuta askari wa vikosi mbali mbali pamoja na madaktari ambapo walipewa taarifa ya kufariki kwa ndugu zao na kutakiwa kuzitambua maiti na kuzichukua kwa ajili ya mazishi lakini alidai wao walikataa kuchukua maiti hao kwa madai kuwa jamaa zao walichukuliwa wakiwa wazima kwa hivyo hawawezi kuwapokea wakiwa maiti. Mzee huyo alidai kuwa wakati wakiendelea kujadiliana, maiti hizo ziliondoshwa na kupelekwa Kiungoni kwa ajili ya mazishi ambapo mtoto wa marehemu anaefanya kazi katika kikosi cha JKU aitwae Rashid alishiriki katika kuandaa mazishi hayo.

Imedaiwa zaidi kuwa maiti hizo zilipelekwa Kiungoni kwa kutumia gari la KVZ lakini askari wa JKU kutoka kambi ya Msaani ndio walioshiriki katika kuchimba kaburi na kusimamia mazishi yote.

Hivyo, Pamoja na hatua zilizoanza kuchukuliwa na Jeshi la Polisi. THBUB inaona kuna mambo kadhaa ya kuchunguzwa kwenye tukio hili.

Itakumbukwa kwamba tukio hili limetokea wakati THBUB inaendelea na kazi ya uchunguzi wa kifo cha watu wawili waliofariki kwa ajili kudaiwa kupigwa risasi na vyombo vya ulinzi na usalama huko Kidoti Mkoa wa Kaskazini Unguja

Hivyo, THBUB inakusudia kufanya uchunguzi wa tukio hili kwa mujibu wa Ibara 130 (1) (c) na (f) ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na kifungu cha 6 (1), c,f,g. Pamoja na kifungu cha 15 (1)

(a) vya sheria ya THBUB Sura ya 391 ili kubaini ukweli wa tukio hili na kama kuna uvunjifu wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora

Aidha, THBUB inapenda kuwakumbusha wananchi na taasisi zote, umuhimu wa kupiga vita vitendo vyote vinavyovunja Sheria na kukiuka misingi ya utawala bora

Mwisho, THBUB inawashukuru wanahabari na wananchi wote waliotoa taarifa kuhusu tukio hili. Pia THBUB inatoa pole kwa kila aliyeathirika na tukio hili na kuwaomba wananchi wote kuwa watulivu na wenye subira hususan katika kipindi hichi ambacho vyombo husika vinaendelea na uchunguzi.

Imetolewa na

……………………………

Khatib M. K. Mwinyichande

Kamishna

**TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA**

**Januari …10…, 2025**